M14/2/ANSWA/SP1/SWA/TZ0/XX/T

22142835

International Baccalaureate®
Baccalauréat International
Bachillerato Internacional

**SWAHILI AB INITIO – STANDARD LEVEL – PAPER 1**
**SWAHILI AB INITIO – NIVEAU MOYEN – ÉPREUVE 1**
**SWAHILI AB INITIO – NIVEL MEDIO – PRUEBA 1**

Tuesday 13 May 2014 (morning)
Mardi 13 mai 2014 (matin)
Martes 13 de mayo de 2014 (mañana)

1 h 30 m

---

TEXT BOOKLET – INSTRUCTIONS TO CANDIDATES

- Do not open this booklet until instructed to do so.
- This booklet contains all of the texts required for paper 1.
- Answer the questions in the question and answer booklet provided.

LIVRET DE TEXTES – INSTRUCTIONS DESTINÉES AUX CANDIDATS

- N'ouvrez pas ce livret avant d'y être autorisé(e).
- Ce livret contient tous les textes nécessaires à l'épreuve 1.
- Répondez à toutes les questions dans le livret de questions et réponses fourni.

CUADERNO DE TEXTOS – INSTRUCCIONES PARA LOS ALUMNOS

- No abra este cuaderno hasta que se lo autoricen.
- Este cuaderno contiene todos los textos para la prueba 1.
- Conteste todas las preguntas en el cuaderno de preguntas y respuestas.


© International Baccalaureate Organization 2014

https://xtremepape.rs/


Blank page
Page vierge
Página en blanco



https://xtremepape.rs/

**MATINI A**

# MALKIA KATIKA MBIO ZA MARATHONI




❶ Keitany ni mwanariadha wa mbio za masafa marefu ambaye amekuwa bingwa katika mbio kadhaa. Watu mwengi humtambua Keitany kama mwanariadha mpole na mnyenyekevu.

❷ Unapokutana naye, tabasamu ndio kitu cha kwanza utakachokutana nacho. Tabasamu lake linaongezeka anapotangazwa bingwa wa marathoni kuu duniani kama *World Marathon Majors*. Kwa ushindi huo wenye mikondo mitano, alituzwa shilingi million arobaini na tatu.

❸ Kisha Keitany alipata taji jingine la mwanamichezo bora wa kike katika tuzo za SOYA hapa nchini akimshinda bingwa wa dunia katika mbio za mita 5000.

❹ Vivian Cheruiyot Keitany alianza kutimuka mbio alipokuwa darasa la nne katika Shule ya Msingi ya Kanjulul kabla ya kuhamia shule ya Kisok wilayani Koibatek.

❺ Alijiunga na Nairobi *Hidden Talent Academy* kwa masomo ya sekondari mwaka wa 2002 na ni hapa ndipo alipoanza mazoezi kabambe ya mbio za mita 1500 na 5000. Alifanya vizuri katika mbio za mita 5000 huku aking'aa hadi kitengo cha taifa.

❻ Binti huyu anajivunia kuwa katika orodha ya mashujaa wa kike duniani kama vile Grete Waitz (1978), Tecla Loroupe (1994), Deen Castor (2001), Marla Runyan (2002), na Kim Smith (2008).

❼ Keitany hakushiriki mbio mwaka wa 2008 kwa sababu alikuwa amejifungua mtoto. Hata hivyo katika mwaka wa 2009, alishinda mbio za *World Half Marathon* mjini Barmingham na mnamo mwaka wa 2011 aliibuka mshindi katika mbio za London.

Benard Rotich, *Taifa Leo* (2012)



https://xtremepape.rs/

**MATINI B**

# NYOTA ZETU

## JE UNGETAKA KUJUA KUHUSU MAISHA YAKO?

**PUNDA: Machi 21 – Aprili 19**



- Leo ni siku nzuri ya urafiki.
- Usijinyime raha.
- Lakini usimpe rafiki yako siri zako za kifedha kwa wakati huu.
- Subiri kwa muda wa kama mwezi mmoja.
- Muda huu ni mrefu na utakuwa umemjua rafiki yako vizuri.
- Huu ndio wakati unaoweza kumwambia siri zako za pesa na mengine ya kibinafsi.

**NG'OMBE: Aprili 20 – Mei 20**



- Badilisha tabia leo.
- Umekuwa mtu wa tamaa.
- Tabia hii itakunyima mambo mengi mazuri.
- Pia umekuwa hushirikiani na wenzako.
- Jua kwamba katika maisha haya ni vyema kushirikiana na wengine.

**MAPACHA: Mei 21 – Juni 21**



- Ulikosana na mtu hivi karibuni.
- Usipange kukutana naye sasa kwa sababu bado ana hasira.
- Lakini usiwe na huzuni kwa haya.
- Panga wakati mzuri wa kuomba msamaha.
- Ukifanya hivi mambo yako yataenda sawa.

**KAA: Juni 22 – Julai 22**



- Mjomba wako atakutumia ujumbe hivi karibuni.
- Ujumbe huu utakuwa wa kukupongeza.
- Pongezi hizi zitatokana na ufanisi wako katika kupata kazi uipendayo.
- Mjomba wako pia atakusaidia katika kujitayarisha kuanza kazi hii.
- Usidharau ushauri wake.

Sheikh Khabib, *Taifa Leo* (2012)



https://xtremepape.rs/

**MATINI C**

# KUHIFADHI MAZINGIRA

Kijiji cha Mpeketoni,
S.L.P. 40050-00200,
LAMU.
20.03.2013.

Afisa wa Mazingira,
S.L.P. 18300-00500,
NAIROBI.

**KUH: <u>KUHIFADHI MAZINGIRA</u>**

❶ Ninachukua nafasi hii kukuandikia ili nikueleze mambo makuu yanayonitatiza katika kijiji chetu. Kabla kukuelezea jambo linalonitatiza, kwanza ningetaka kukupongeza kwa bidii zako katika kuhifadhi mazingira. Kwa kweli, wewe, afisi yako pamoja na wenzako wa idara ya kuhifadhi mazingira, mmesaidia pakubwa kuhahakisha kuna hali nzuri ya usafi katika mazingira yetu. Sijui nikupongeze vipi? Hata hivyo nakupa hongera nyingi kwa bidii zako.

❷ Siku ya leo tena ninayo huzuni kubwa kukufahamisha kwamba mazingira yanachafuliwa kwa mara nyingine. Mimi nikiwa kiongozi wa shughuli za kulinda mazingira na usafi, nimehuzunika sana na vitendo vya ajabu vya watu wengine kutoka usiku usiku na kwenda kutupa takataka na uozo wa kila aina mahali popote bila kujali.

❸ Zaidi ya hayo, juzi wafisadi wengine walikata misitu yetu. Walikata miti yote iliyokomaa na kwenda kuiuza. Miti hiyo inatumiwa kutengenezea fenicha huku vijijini. Ukataji huu wa miti ndio unaoendeleza ukame katika sehemu hizi zetu. Jangwa hili linachangia mmomonyoko wa udongo na uharibifu wa mazingira yetu.

❹ Ninakuomba ututumie huduma nyingine tena. Kumbuka atafutaye hachoki. Tafadhali tuletee malori ya kuzoa takataka hizi zilizojazana mitaani na barabarani. Pamoja na hayo, tunaomba ulinzi na usalama wa wafanyikazi wa pori kwa ajili ya misitu na miti yetu. Hayo yatakapofanyika, mazingira yetu tutaweza kuyahifadhi vyema.

Wako mwaminifu,

Mpasua msonobari

Kiongozi wa kijiji.

W Wallah, *Kiswahili Mufti: Darasa la Saba* (2001)



https://xtremepape.rs/

**MATINI D**

# ARUSI PEMBA

*Nyaruganda ni mwanamke Mganda ambaye amezuru eneo la Pemba pamoja na mumewe kwa likizo ya mapumziko. Wameishi Pemba kwa muda wa mwezi mmoja sasa. Wamekuwa wakiishi na familia moja ya Mzee Kututwa Mohamed. Yafuatayo ni mazungumzo yaliyojiri wakati mmoja baina ya mke wa Mzee Kututwa, Zeinabu na Nyaruganda.*

**Zeinabu**: Nakualika kwa ngoma kesho kutwa.

**Nyaruganda**: Aaah!! Asante! Je, naweza kuja na mume wangu?

**Zeinabu**: La hasha! Mume wako haruhusiwi kuja ngomani. Hii ni ngoma ya wanawake pekee.

**Nyaruganda**: Lahaula! Haya niambie ni ngoma gani hii ambayo ni ya wanawake pekee?

**Zeinabu**: Hii ni ngoma ya arusi. Bi. arusi atakuwa anapewa mawaidha kwao nyumbani kabla ya kwenda kwa mumewe. Baada ya mawaidha ndio ngoma itakapoanza. Ngoma mbalimbali zitachezwa kama chakacha, lelemama na vugo.

**Nyaruganda**: Alaa! Na bibi arusi mwenyewe ni nani?

**Zeinabu**: Ni binti ya Mzee Bakari, yule jirani yetu kule mashambani. Mzee ambaye ana shamba kubwa sana la karafuu.

**Nyaruganda**: Aaah! Ninamjua msichana huyu. Alikuja hapa wakati mwingine ili kutujulisha kuhusu maleso ya arusi.

**Zeinabu**: Ndio, ni yeye. Kumbe unamjua. Basi huyo ndiye bibi arusi.

**Nyaruganda**: Na ni mvulana yupi aliyebahatika kumwoa?

**Zeinabu**: Bwana arusi ni Rashid, mtoto wa wifi yangu, dadake mzee Kututwa.

**Nyaruganda**: Nipashe mengi zaidi kuhusu arusi hiyo!

**Zeinabu**: Kwa hivi sasa bibi arusi amekuwa hatoki nyumbani kwa wiki mbili. Amekuwa akirembeshwa kwa kusingwa liwa!

**Nyaruganda**: Ehe! Niambie! Ni mambo ya kushangaza!



https://xtremepape.rs/

**Zeinabu**: Haya si ya ajabu. Ni mambo ya kawaida kwetu! Wakati huu wa wiki mbili pia bibi arusi amekuwa akikaa na shangazi yake na kila siku anapewa mawaidha ya jinsi ya kuishi na mume.

**Nyaruganda**: He! Yarabi!

**Zeinabu**: Usishtuke Nyaruganda. Hizo ndizo mila zetu.

Kwa hivyo kabla ya ngoma kuanza, bibi arusi ataoshwa na shangazi yake kisha arembeshwe kwa kupakwa henna, wanja na rangi ya mdomo. Kisha atavikwa vazi lake la arusi na abebwe mgongoni na shangazi yake kama mtoto hadi uwanja wa ngoma.

**Nyaruganda**: Halafu? Nina hamu ya kujua zaidi!

**Zeinabu**: Halafu huyo shangazi yake atampa mawaidha ya mwisho hapo hadharani. Kisha wengine watapewa nafasi ya kutoa mawaidha yao. Baada ya haya ngoma itaanza. Ngoma itakayoanza ni chakacha. Bibi arusi anatakikana afungue ngoma hii kwa kucheza na kuonyesha ubingwa wake wa kuzungusha kiuno kama kwamba hana mifupa. Wengine watajiunga naye kwa kusakata vilivyo. Kisha ngoma ya lelemama itafuata. Ngoma hii itaendelea hadi chee! Ngoma itakayomsindikiza bibi harusi kwa mumewe ni ya vugo ambayo itakuwa mwendo wa asubuhi. Kwa ufupi hivi ndivyo mambo yatakavyokuwa.

**Nyaruganda**: Aaaa rafiki! Nina hamu sana kuhudhuria sherehe hii. Utamaduni wa Waswahili wa Pemba unapendeza na bado unafuata ya mambo ya kale. Kule kwetu Uganda mambo ni tofauti. Nitakualika siku moja pia uje ujionee.

**Zeinabu**: Asante dadangu. Wacha twende tukajitayarishe ili tuanze safari ya arusini.

Nancy Jumwa Ngowa, *Arusi Pemba* (2013)



https://xtremepape.rs/